MUHTASARI WA MKUTANO MAALUMU WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA TAREHE 05/08/2017.

A: WAJUMBE WALIOHUDHURIA:

1.	Mh. Namkulya S. Namkulya	-Kata ya Mihambwe	- Mwenyekiti
2.	" Jamal M Mtima	-Kata ya Namikupa	- M/Mwenyekiti
3.	" Katani A. Katani	-Mbunge- Tandahimba	-Mjumbe
4.	" Issa Nasoro Kalumbe	-Kata ya Mahuta	"
5.	" Ngerezani Bakari Musa	-Kata ya Kitama	"
6.	" Kawasaki Lipangati	-Kata ya Mnyawa	"
7.	" Simba Nasoro Hashimu	-Kata ya Naputa	"
8.	" Chimale S. Abdallah	-Kata ya Lukokoda	"
9.	" Sharafi Dihoni Hamisi	-Kata ya Malopokelo	"
10.	" Mtimbuka K.Ramandani	-Kata ya Nambahu	"
11.	" Mawazo S. Mbombenga	-Kata ya Nanhyanga	"
12.	" salumu Makuyeka	-Kata ya chikongola	"
13.	" Ally D. Nantindu	-Kata ya Michenjele	"
14.	" Nembo H. Mchola	-Kata ya Maundo	"
15.	" Ahmadi A. Ndende	-Kata ya Mkoreha	"
16.	" Ashura m. Ngope	-Kata ya Mchichira	"
17.	" Mohamedi T. Ussi	-Kata ya Kwanyama	"
18.	" Selemani Y. Chambengela	-Kata ya Litehu	"
19.	" Ismail S. Chipoka	-Kata ya Ngunja	"
20.	" Zainabu H. Mpota	-Kata ya Mkonjowano	"
21.	" Alafa T. Nakatanda	-Kata ya Mkwiti	"
22.	" Ayubu Mohamedi	-Kata ya Lyenje	"
23.	" Rashidi N. Mtima	-Kata ya Chingungwe	"
24.	" Mfaume H. Abdallah	-Kata ya Miuta	"
25.	" Mkwahe M. Milembu	-Kata ya Chaume	"
26.	" Salumu A. Mnyongo	-Kata ya Dinduma	"
27.	" Abdallah H. Ponela	-Kata ya Luagala	"
28.	" Likapa J.Nangololo	-Kata ya Mndumbwe	"
29.	" Hamisi B. Nayowela	-Kata ya Tandahimba	"
30.	" Fakihi M. Mwango	-Kata ya Mdimba	"
31.	" Yusufu B. Nampoto	-Kata ya Mkundi	"
32.	" Asha R. Tebwa	-Viti Maalum	"
33.	" Halima Tamatama	-Viti Maalum	"
34.	" Huduma S. Mnoda	-Viti Maalum	"
35.	" Amina Issa Mpota	-Viti Maalum	"
36.	" Hadija S. Mnihwika	-Viti Maalum	"
37.	" Shamia M. Kaisi	-Viti Maalum	"
38.	" Fidea A. Hittu	-Viti Maalum	"
39.	" Asia A. Likoba	-Viti Maalum	"

40. “ Rehema C. Liute -Viti Maalum “
41. “ Hawa M. Ramandani -Viti Maalum “
42. “ Amina A. Simba -Viti Maalum “

B: WASIOFIKA

1. Mhe. Ramadhani Ulaya -Kata ya Milongodi -Amefariki

C:WAKUU WA IDARA NA VITENGO WALIOHUDHURIA

1. Ndg Said A. Msomoka - Mkurugenzi Mtendaji (W) Katibu
2. Ndg. Ahmada Suleiman - Afisa Utumishi (W)
3. “ Machela A.H -Mweka Hazina (W)
4. “ Issa Naumanga -Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W)
5. “ Hassani Msangawenga -Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)
6. Eng: Peter Malekia - Mhandisi wa Maji (W)
7. Dr. Antipas Swai -Mganga Mkuu (W)
8. Ndg: Bibiana Molenga -Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii(W)
9. “ Nassib N. Shaibu -Kaimu Afisa Ardhina Maliasili(W)
10. “ Robert Mwanawima -Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
11. “ Lazaro Matoke - Kaimu Afisa Uchaguzi
12. “ Sosteness Luhende -Afisa Elimu Sekondari (W)
13. “ Abdilah Mfinanga - Afisa Mipango (W)
14. “ William Kongola -Mkaguzi wa ndani wa Hesabu(W)
15. “ Rajabu Lwazi -TEO- Mahuta
16. “ Nosyaga Mwailunga - Kaimu Afisa Usafi na Mazingira(W)
17. “ Rajabu C. Athman -Afisa Utamaduni
18. “ Hadija Mwinuka -Afisa Elimu msingi(W)
19. “ Zuberi Sarahani -Mwanasheria
20. “ Protas Muhanuzi -Afisa Manunuzi(W)
21. “ Ismail Mbilinyi -Mratibu wa TASAF
22. “ James C. Chitumbi -TEO Tandahimba
23. “ Joseph Mongi - Afisa TEHAMA
24. “ Constantine Kasese - Afisa Mipango

D: WAALIKWA

1. Mh: Halima Ndendego - Mkuu wa Mkoa Mtwara
2. Mh. Sebastian Waryuba -Mkuu wa Wilaya Tandahimba
3. Luteni col. Elvis Massawe - Mshauri Mgambo(M)
4. Luten Col. Valentine Makyao - Afisa wa Jeshi la Wananchi
5. Ndg: Mohamedi Mtama -Mshauri wa Mgambo(W)
6. “ Frentirine Tesha -Mkuu wa Polisi (W)
7. “ Thomas Mhecha -Afisa Usalama (W)
8. “ Raymond Mapunda - Kaimu Afisa Uhamiaji(W)
9. “ Deogratius Mbowe - Kamanda wa TAKUKURU(W)

10. " Salumu Masalanga - Afisa Elimu(M)
11. " Huko Njau -Mkaguzi wa Hesabu(M)
12. " Tonido Mbabele - Mkaguzi wa Hesabu
13. " Mdedemu Ibrahimu - Mkaguzi W hesabu
14. " Kilapilo charles -Ofisi ya RAS Mtwara
15. " Mohamedi Wasinde -Afisa Serikari za Mitaa
16. " Paul Shamweta -Mhasibu
17. " Nuru Ringo -Afisa Serikali za Mitaa(M)
18. " Thomasi Limbila -Ofisi ya Mkaguzi wa Hesabu (CAG)
19. " Mwajuma kwipunda - Ofisi ya Mkaguzi wa Hesabu (CAG)
20. " Mkunda Chilunga - Ofisi ya Mkaguzi wa Hesabu (CAG)
21. " Edith Shayo - Ofisi ya RAS Mtwara
22. " Tabitha Kilangi - Ofisi ya RAS Mtwara
23. " Amani Lusake -Ofisi ya RAS Mtwara
24. " Evaristi masuha -Ofisi ya RAS Mtwara
25. Eng: Paul Mlia -Meneja TARURA(W)
26. " Juma A. Lusasi -Afisa Tarafa Mahuta
27. " Rehema Hoza -Afisa Tarafa Litehu
28. " Born Minga -Afisa Tarafa Namikupa
29. Mbaraka Hittu -Katibu CUF (W)
30. " Willy Mkapa -Katibu CHADEMA (W)
31. " Namtula A. Haji - Mwenyekiti CCM(W)
32. " Domina A. Soko -Katibu CCM (W)

E: SEKRETARIATI

1. Christian Mazuge
2. Sofia Nanjota
3. Mohamedi Namkuva

MUHT.NA. 01/2017/2018- KUFUNGUA MKUTANO

Katibu alieleza kuwa huu ni mkutano maalum kwa ajili ya Kujadili Taarifa ya Mkaguzi na mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kisha alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao.

Mwenyekiti aliwakaribisha Wajumbe,Wageni waalikwa na watendaji katika Mkutano huo Maalum na alifungua kikao saa 5: 10 asubuhi.

MUHT.NA. 02/2017/2018- TAARIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI YA UKAGUZI WA HESABU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016.

HOJA ZA UKAGUZI:

Mweka Hazina(W) aliwasilisha taarifa ya mkaguzi na mdhibiti Mkuu wa hesabu za serikali juu ya ukaguzi wa hesabu za Halmashauri ya wilaya ya Tandahimba za mwaka wa fedha unaoishia 30,Juni 2016.

Kwa mujibu wa taarifa ya ukaguzi wa hesabu kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ilipata **Hati Safi.** Ukaguzi huu ni kwa miradi ya Jumla na pamoja na miradi ya Afya,Maji,barabara na kilimo.

Hata hivyo kulikuwa na mapendekezo 48 ya mwaka 2015/2016, 22 ya mwaka 2013/2014 na 21 ya mwaka 2013/2014 yaliyohitaji majibu ya menejimenti. Menejimenti ilijibu kuwa mapendekezo yote ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na hoja zinazotokana na ukaguzi wa nyuma ambapo hoja 11 za nyuma zilifungwa na kubakiwa na hoja 37, hoja 3 za mwaka 2014/205 zilifungwa na kubakiwa na hoja 19 na hoja 10 za mwaka 2013/2014 zilifungwa na kubakiwa na hoja 11.Vilevile hoja 4 za mwaka 2014/2015 zilipitwa na matukio na baadhi ya hoja zitahakikiwa wakati wa ukaguzi ujao.

Menejimenti inaendelea kufanya juhudi za kuhakikisha inajibu hoja ambazo hazijafungwa na kuwasilisha majibu kwa mkaguzi kwa ajili ya uhakiki.
Taarifa ilipokelewa na Wajumbe.

MAJADILIANO:

MAPATO YA NDANI AMBAYO HAYAKUKUSANYWA.

Ilielezwa kuwa Halmashauri Ilikisiwa kukusanya Jumla ya shilingi 3,973,334,350/= kama mapato ya ndani hata hivyo iliweza kukusanya shilingi 3,553.854,839 na hivyo kuwa na naksi ya shilingi 419,479,511/= sawa na asilimia 11. Menejimenti ilieleza kuwa imeanza kukusanya mapato kwa kubuni vyanzo vipya kama vile Ada ya kuegesha malori,Ada ya uchimbaji madini ya ujenzi na ushuru wa mabango. Wajumbe walisisitiza menejimenti kuongeza nguvu ya ukusanyaji wa mapato kikamilifu.

MADAI

Ilielezwa kuwa hadi kufikia Juni. 30 .2016 Halmashauri ilikuwa na madai ya shilingi 2,046,983,584.00. Hivyo mkaguzi alitilia shaka uwezo wa menejimenti juu ya ukukusanyaji wa madeni.

Ilielezwa kuwa kuna utaratibu wa kufuata madeni hayo kwa yale ambayo hayaoneshi mwelekeo wa kulipa kwa kufuata sheria na kanuni za serikali. Ilielezwa kuwa menejimenti ipo kwenye mchakato wa kuwasilisha mapendekezo ya kufuta baadhi ya madeni.

USHAURI.

Mkuu wa Mkoa alieleza kuwa madeni hayo yasifutwe bali yalipwe hata kama ni kwa awamu.

AZIMIO.

1. Mkakati wa kudai madeni uandaliwe na uwasilishwe kwenye Baraza la kawaida sawa na mkakati wa kudai Vyama vya Msingi.

MASHAURI YA HALMASHAURI

Ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 Halmashauri ilikuwa na shauri moja ambapo Halmashauri ndio Mshitakiwa ambalo ni la Highchem (T) LTD V/S Bodi ya Korosho Halmashauri Ilijibiwa kuwa Mzabuni alisambaza Pembejeo bila kibali cha Halmashauri na pia alisambaza kiasi zaidi ya mgao wa Halmashauri.

USHAURI

Halmashauri ifanye ufuatiliaji wa karibu hadi pale kesi itakapokamilika.

MAGARI 11 MABOVU

Ilielezwa kuwa wakati ukaguzi unafanyika ilibainika kuwepo kwa magari 11 mabovu yaliyotelekezwa**.**

Ilijibiwa kuwa magari hayo yaliombewa kibali cha kuuzwa na yalitakiwa kukaguliwa na TEMESA ndipo yapate idhini ya kuuzwa. Kwa sasa menejimenti inawasiliana na TEMESA ili wafanye ukaguzi.

MAGARI 3 YASIYO NA BIMA

Ilielezwa kuwa kwa mujibu wa kifungu Namba 95 (1) cha waraka wa fedha za Serikali za Mitaa inaeleza kuwa magari ya Halmashauri inabidi yakatiwe bima kulingana na sheria na mahitaji ya Halmashauri**.**

Ilielezwa kuwa kumekuwa na ugumu wa kupata bima kwa magari ya STK na DFP. Ilielezwa kuwa ufuatiliaji ufanyike kwa kuzingatia ushauri wa mkaguzi wa Mkuu wa Hesabu za Serikali na utaratibu wa Wizara.

MAKUSANYO YA CHINI YA USHURU WA MAZAO KUTOKA KATIKA BEI YA SOKO.

Ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 Halmashauri ilikusanya ushuru kwa kutumia bei dira. Kinyume na kifungu cha 7(1) g cha sheria ya fedha za serikali za mitaa ya mwaka 1982.

Mwanasheria alieleza kuwa wanasheria wa Mtwara waliandika barua kwa Mkurugenzi wa Bodi ya korosho juu ya kubadili utaratibu wa mauzo ya korosho na kuahidi kufungua kesi Mahakamani ili Halmashauri zipate stahiki zake.

Maoni ya Baraza

Kesi ifunguliwe ili Halmashauri ipate mapato yake stahiki. Mwanasheria afungue kesi tarehe 7/8/2017.

Mkuu wa Mkoa alieleza kuwa Mkoa unatoa Baraka zote kesi ifunguliwe kwani sheria zilipandishwa kwa maslahi ya watu wachache.

MATUMIZI YA FEDHA ZA MFUKO WA PEMBEJEO KULIPA POSHO

Ilielezwa kuwa fedha za mfuko wa pembejeo zilitumika kulipa posho kwa zaidi ya asiliamia 50 kinyume cha mwogozo na maelekezo katika mwaka wa fedha 2015/2016..

Mkuu wa Mkoa alieleza kuwa fedha hizo zitumike kuendeleza zao la korosho kwa kuhamasisha, mafunzo. Aliahidi kuwasiliana na Bodi ya korosho kubadili miongozo ya matumizi ya fedha hizo ili ziendane na mahitaji halisi.

KUTOKUANDALIWA KWA TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA AFYA YA JAMII.

Ilielezwa kuwa wakati ukaguzi unafanyika ilibainika kuwa bodi ya Mfuko wa Afya ya Jamii haikutayarisha Taarifa ya mapato na matumizi kinyume cha kifungu Namba 9 cha sheria ndogo.

Maoni ya kamati:

Hoja isijirudie tena kwani wataalam wa kuandaa taarifa hizo wapo.

MCHANGO WA HALMASHAURI KWA MFUKO WA MAENDELEO YA WANAWAKE NA VIJANA

Ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 Halmashauri ilikusanya shilingi 3,553,854,839.00 za mapatto ya ndani. Hata hivyo shilingi 192,000,000/= zilitolewa kwa ajili ya vikundi vya wanawake na vijana badala ya 355,385,483.90 na hivyo kuacha salio la shilingi 163,385,483.90.

USHAURI

Mkuu wa Mkoa alishauri kila mwezi 10% ya vijana na wanawake itengwe kabisa kabla ya kufanya matumizi.

Maoni ya Baraza

Suala la kutenga 10% kila mwezi litafanyiwa kazi kwenye Mfuko wa vijana na wanawake.

KODI YA ARDHI

Ilielezwa kuwa wakati wa ukaguzi jumla ya shilingi 33,048,505.14 zilikusanywa kama kodi ya Ardhi kwa niaba ya Wizara ya Ardhi lakini hazikutumwa kwenda Wizara ya Ardhi,Maendeleo ya Nyumba na Makazi kinyume na mwongozo wa serikali ambao unaitaka Halmashauri kutuma fedha hizo na baadae kurejeshewa asilimia thelathini (30%) ya mapato.

USHAURI

Ufuatiliaji ufanyike ili kupata mwongozo mpya wa Wizara kutokana na mabadiliko yaliyofanywa na Wizara.

UHABA WA MIUNDOMBINU YA ELIMU

Ilielezwa kuwa wakati ukaguzi unafanyika ilibainika kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ina uhaba wa miundombinu katika shule za Msingi na Sekondari pamoja na Vifaa vya maabara.

Maoni ya Baraza

Vifaa vinunuliwe na utunzaji ufanyike ili 2017/2018 ikiwezekana kompyuta zinunuliwe Kwa ajili ya kujifunzia wanafunzi.

SHIMO YA MCHANGA LUKOKODA

lielezwa kuwa shughuli za kijamii na kiuchumi zinazofanyika wilaya ya Tandahimba zimesababisha kuwepo kwa shimo kubwa ambalo halijafukiwa hadi wakati ukaguzi unafanyika.

KUCHELEWA KUTUMWA KWA FEDHA

Katika mwaka wa fedha 2015/2016 halmashauri ilipokea Jumla ya shilingi 329,607,000/= kwa ajili ya kugharamia shughuli za mfuko wa pamoja(Basket Fund) kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Lakini shilingi 164,803,500/= zilipokelewa mwishoni mwa mwezi June, 2016.

Ushauri

Baraza lilishauri miradi ambayo haijatekelezwa, itekelezwe mwaka wa fedha 2017/18

KASI NDOGO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI .

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ina miradi minne ya maji inayoendelea kutekelezwa kwa ajili ya kutoa huduma ya maji. Hata hivyo wakati ukaguzi unafanyika ilibainika kuwa miradi ina zaidi ya miaka miwili tangu iaze kutekelezwa kinyume cha muda wa makubaliano yaliyopo kwenye mkataba.

MAONI YA BARAZA

Utekelezaji wa miradi ya maji ufanyike kwa kasi ili wananchi wapate huduma ya maji.

MALIPO YASIYO STAKABADHI ZA KIELEKTRONIKI

Katika mwaka wa fedha 2015/2016 halmashauri ilifanya malipo kwa kutumia mfuko wa barabara kiasi cha shilingi 381,250,537.40 bila kudai risiti za kielektroniki kinyume cha sheria ya kodi ya mapato. Menejimenti ilieleza kuwa ilifanya malipo hayo kwa kuwa watoa huduma wengi hawakuwa na risiti za kielektroniki.

USHAURI

Orodha ya watoa huduma ipelekwe Mamlaka ya mapato nchini (TRA) ili hoja ifungwe.

UENDESHAJI WA MRADI WA UMWAGILIAJI LITEHU.

Halmashauri ilianzisha mradi wa umwagiliaji Litehu uliogharimu shilingi **691,989,250/=** sawa na **63%** ya gharama yote ya mradi shilingi **1,100,00,000.00.** ukaguzi ulipofanyika uligundua kuwa uzalishaji wa mazao haufanyiki, eneo la hekta 260 halitumiki kwa uzalishaji. Mpunga unaovunwa ni tani 2.1 badala ya tani 4.5 kwa hekta. Menejimenti ilieleza kuwa itaongeza juhudi za

kuwahamasisha wananchi wazalishe mpunga kupitia mradi wa umwagiliaji wa Litehu.

USHAURI

Mkuu wa mkoa alishauri kuwa Mradi unatakiwa ufanye kazi sawa na kiasi cha fedha kilichowekezwa na kushauri waheshimiwa Madiwani kufanya ufuatiliji wa miradi hiyo.

NASAHA ZA MKKUU WA WILAYA

Mkuu wa wilaya alipongeza Halmashauri kwa kufanya kazi kwa uadilifu na kujituma na kushauri kufanya kazi kwa bidii ili kuongeza kasi ya maendeleo.

MKUU WA MKOA

Alipongeza Halmashauri kwa kupata **Hati Safi** katika mwaka wa fedha 2015/2016 na kueleza kuwa hoja nyingi zilizoibuliwa ni za kisera .

USHAURI

Ukaguzi wa ndani uzuie hoja kwa kupitia kwa makini kila robo. Alipongeza pia halmashauri kwa kuvuka makisio ya mapato na kuhimiza ushirikiano kwa Madiwani.

Suala la kuchelewa kwa fedha za Serikali kuu aliahidi kutoa ushirikiano kulifanyia kazi.

Suala la tozo za ushuru wa Korosho aliahidi kutoa ushirikiano ili kufanikisha suala hilo

Katibu alishukuru kwa nasaha na kueleza kuwa lami inayojengwa Tandahimba inatokana na mapato ya ndani tofauti na Halmashauri zingine ambazo zinazotegemea ruzuku kutoka serikali kuu au wafadhili.

MUHT.NA.03/2017/2018 - KUFUNGA MUKUTANO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na kueleza kuwa suala la mfuko wa wanawake na vijana linapaswa kulifanyia kazi. Pia alisema suala la barabara ya lami jitihada zitaongezwa ili kuhakikisha mtandao wa lami unaongezwa na kisha alifunga Mkutano saa .07: 10 mchana.

MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA

JINA _____ **JINA** _____

MWENYEKITI **KATIBU**

SAINI _____ **SAINI** _____

_____

TAREHE